

SABATO

Je, Sabato Ilikoma kwa Kuwa Ilikuwa Kivuli cha Mambo Yajayo?

Kuna mafundisho yanayoenea kwamba Sabato ilikuwa ni kivuli cha mambo yajayo, na hivyo haina tena umuhimu kwa Wakristo. Wengine hudai kwamba kwa kuwa Kristo amekuja,...

PR. ALMODAD AMOS YARAGWILLER

2026

Kuna mafundisho yanayoenea kwamba Sabato ilikuwa ni kivuli cha mambo yajayo, na hivyo haina tena umuhimu kwa Wakristo. Wengine hudai kwamba kwa kuwa Kristo amekuja, hakuna haja tena ya kuitunza. Hoja hii imekuwepo muda mrefu, lakini sasa inapoanza kutolewa hata na baadhi ya wahubiri wanaojulikana kama watunzaji wa Sabato, inakuwa ni muhimu sana kufafanua tena tofauti iliyopo kati ya **Sabato ya Uumbaji**, ambayo ndiyo tunayoitunza leo, na zile **Sabato nyingine** zilizokuwa sehemu ya sikukuu za Maadhimisho wakati wa Agano la Kale.

Asili ya Sabato

Kwanza kabisa ni muhimu kuelewa Sabato ni nini: Sabato ni siku ya saba ya juma, muda maalum ulitengwa na Mungu (Mwa. 2:1-3) kwa makusudi ya Ibada (Lk. 4:16), ili kuitumia siku hiyo kuwa kumbukumbu ya uumbaji (Kut. 20:9-10) na kumbukumbu ya ukombozi (Kumb. 5:15). Sabato ya kwanza haikutokana na mfumo wa kafara au ibada za Musa. Ilianzishwa na Mungu mwenyewe **mwanzoni mwa historia ya dunia**. Biblia inasema:

> “Na Mungu alipomaliza kazi yake siku ya saba, akapumzika siku ya saba... Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa.” (Mwanzo 2:2–3)

Hapa ndipo Sabato ilipoanza — **kabla ya dhambi, kabla ya Wayahudi, kabla ya dini yoyote**. Iliwekwa ili mwanadamu akumbuke kazi ya uumbaji wa Mungu. Kwa hiyo, Sabato hii **ni kumbukumbu ya jambo lililotokea tayari huko nyuma**, si kivuli wala kielelezo cha jambo ambalo lingetokea huko mbeleni.

Zaidi ya hapo, Mungu mwenyewe alisema Sabato ni **ishara ya uhusiano kati yake na watu wake**:

> “Tazama, nalitoa Sabato zangu ziwe ishara kati ya mimi na wao, wapate kujua ya kuwa mimi ndimi Bwana niwatakasaye.” (Ezekieli 20:12).

Hivyo, Sabato ya siku ya Saba inayokuja kwetu katika kila juma ni **kumbukumbu ya uumbaji** na **ishara ya kazi kubwa ya kati ya utakaso** ambayo Mungu ameifanya na anaendelea kuifanya ndani yetu. Kuitunza Sabato ni matokeo ya kuwa Mungu anafanya kazi ya utakaso ndani yako.

Sabato iliongezewa maana ya pili hapo baadaye

Wakati Mungu aliwakomboa Waisraeli kutoka utumwani Misri, aliwakumbusha Sabato ile ile ya uumbaji, lakini akiongeza maana ya pili — **ukombozi**.

Mungu alisema:

> “Kumbuka ya kuwa ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri, naye Bwana Mungu wako alikutoa huko kwa mkono wenye nguvu na kwa mkono ulionyooshwa; kwa hiyo Bwana Mungu wako amekuamuru uitunze siku ya Sabato.” (Kumbukumbu la Torati 5:15)

Kwa hiyo, Sabato ya juma la saba **ni ukumbusho wa mambo mawili makuu**:

1. Kazi ya Uumbaji (Mwanzo 2:2–3)
2. Kazi ya Ukombozi (Kumbukumbu 5:15)

Hapa tena mara nyingine, aina hii ya Sabato tunayoitunza leo ni kumbukumbu ya yaliyotokea — **si kivuli cha mambo ambayo yangekuja hapo baadaye.** Inaonyesha nguvu za Mungu katika kuumba na katika

kukomboa pia. Kwa maneno mengine, Sabato ni **ukumbusho wa yaliyokamilika**, si unabii wa kitu kinachokuja.

Kivuli cha Mambo Yajayo ilikuwa ni nini?

Tofauti na Sabato ya juma la saba, Biblia ilitaja pia **sabato nyingine** zilizokuwa sehemu ya mfumo wa ibada wa Waisraeli chini ya sheria za Musa. Hizi zilihusiana na sikukuu mbalimbali kama vile:

Sikukuu ya Pasaka,

Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu,

Sikukuu ya Majuma (Pentekoste),

Sikukuu ya Upatanisho,

na Sikukuu ya Vibanda.

Katika kila sikukuu, kulikuwa na “sabato” au siku maalum ya pumziko.

Kwa mfano, Biblia inasema:

> “Siku ya kumi ya mwezi wa saba ni Siku ya Upatanisho; ni sabato ya mapumziko.” (Mambo ya Walawi 23:27, 32)

Sabato hizi **hazikuhusiana na uumbaji**, bali zilikuwa **ishara za mambo yajayo**, zikielekeza kwa kazi ya Yesu Kristo.

Ndiyo maana mtume Paulo aliandika:

> “Mtu asiwahukumu kwa chakula, au kinywaji, au kwa sehemu ya sikukuu, au mwezi mpya, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo, bali mwili ni wa Kristo.” (Wakolosai 2:16–17)

Hizi ndizo **sabato zilizokuwa kivuli cha mambo yajayo**, kwa sababu zilitabiri kazi ya Kristo ya ukombozi na upatanisho kupitia msalaba, hapo baadaye. Sabato hizi zilitimia kupitia kifo chake, na **zikakoma, ndiyo maana siku hizi hatuna sikukuu za upatanisho au sikukuu za kutikisha miganda, na nyingine nyingi zilizofanana na hizo**.

Tofauti ya Sabato na Sabato

Sabato ya juma la saba ni ya kipekee kwa sababu **inasimama juu ya mambo yaliyokwisha kutendeka**, si mambo yanayotarajiwa kutokea.

Sabato hii ni **ukumbusho** wa uumbaji na ukombozi — kazi ambazo Mungu amezimaliza.

Ni ishara ya kwamba tumepumzika katika kazi yake iliyokamilika, tukitambua kwamba Yeye ndiye Muumba na Mkombozi wetu.

Sabato nyingine, zile za sikukuu, zilikuwa **kivuli** cha mambo yaliyokuwa bado hayajatimia.

Ziliashiria ujio wa Kristo, dhabihu yake, kifo chake, na kazi yake ya upatanisho.

Zilikuwa kama kivuli kinachoonyesha picha ya kitu halisi kilichokuwa kija.

Lakini Sabato ya Uumbaji haikuwa kivuli cha kitu chochote — ilikuwa **mshahara wa kazi iliyokwisha fanyika.**

Kwa maneno mengine:

Sabato ya siku ya saba ni kumbukumbu ya "Mungu aliumba" na “tumeshakombolewa.”

Sabato za kivuli zilitazamia “tutakombolewa.”

Hapo ndipo tofauti kubwa ilipo.

Yesu Alitunza Sabato na Mitume Waliitunza Sabato pia

Yesu mwenyewe aliiheshimu Sabato hii kama desturi yake:

> “Akaingia katika sinagogi siku ya Sabato kama desturi yake.” (Luka 4:16)

Na hata baada ya kifo na kufufuka kwake, wanafunzi waliendelea kuitunza:

> “Paulo akaingia ndani yao, kama desturi yake, akasema nao kwa maneno ya maandiko kila Sabato.” (Matendo 17:2)

Kama Sabato yote ingekuwa kivuli kilichotimia, Yesu asingeliendelea kuitunza, wala wafuasi wake wasingeifanya kuwa desturi hata baada ya msalaba.

Hii inaonyesha wazi kwamba Sabato ya siku ya saba **haikubatilishwa**.

Sabato: Alama ya Uumbaji na Ukombozi

Sabato inabeba ujumbe wa kudumu wa utambulisho wa Mungu, kwamba Yeye ndiye muumbaji wetu na Mkombozi wetu. Kwa kuitunza, tunakiri kwamba Mungu ndiye Muumbaji wetu na Mkombozi wetu. Ndiyo maana hata katika ulimwengu mpya, Biblia inasema:

> “Na itakuwa kwamba kila mwezi mpya, na kila Sabato, wanadamu wote watakuja kumsujudia mbele zangu.” (Isaya 66:23)

Hivyo Sabato si kivuli cha mambo yajayo, bali ni **ishara ya milele ya uhusiano wa Mungu na viumbe vyake.**

Hitimisho

Sabato tunayoitunza leo si kivuli cha mambo yajayo. Ni **kumbukumbu ya mambo yaliyokwisha kutendeka** — kazi ya uumbaji na kazi ya ukombozi. Hizi ni nguzo mbili muhimu sana zinazotuunganisha na Mungu wetu.

Sabato zilizokuwa kivuli (za wakati wa Agano la Kale) zilielekeza kwa Kristo na zikakoma alipokamilisha kazi yake ya ukombozi msalabani.

Lakini Sabato ya siku ya saba ya kila juma, bado inaendelea kuwa **ishara ya kudumu ya Muumba**, siku maalum ya Ibada, na Amri ya Mungu ambayo ni kumbukumbu ya upendo wa Mungu usiobadilika.

Zaidi kutoka Injili Milele

Makala, vitabu, video na sauti zaidi zinapatikana kwenye maktaba ya Injili Milele:

Sanduku la Agano: Je, Litaonekana Tena?
Unabii · PDF

Nini Hasa Maana ya Kibiblia ya Maneno ya Baba: “Mimi Leo Nimekuzaa”?
Uungu · Video

Je, Yesu ni “Mungu Mwana” au “Mwana wa Mungu”?
Uungu · Video

Kwa Nini Mungu Alimuumba Lusifa?
Pambano Kuu · PDF

Papa Gregory XIII Alipobadilisha Kalenda: Siku Zilivurugwa, Sabato Ilipotea?
Sabato · PDF

Je, ni Lazima Kupiga Magoti Wakati wa Maombi?
Ibada · PDF

Injili Milele

almodad-2.github.io/injili-milele/sw/

WhatsApp +255 718 834 621 · modaofhope@gmail.com

© 2026 Pr. Almodad Amos Yaragwiller · Injili Milele. Haki zote zimehifadhiwa. Usiuze nakala hii bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi.